# MEDALA HIGH SCHOOL

"Discipline for Academic Excellence"

Kitandalu, Idodi - Iringa District, P.o Box 859, Iringa Tanzania
Phone: +255 736 313 180/ +255 735 313 180/ +255 715 817 236
www.medalahighschool.ac.tz/info@medalahighschool.ac.tz


## YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MEDALA MWAKA 2024

**MZAZI /MLEZI WA ……………………………………………………………………..**
**FOMU NAMBA______________**

Napenda kukujulisha kuwa mtoto wako amefaulu mtihani wa usaili wa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule yetu na hivyo amepata nafasi ya kujiunga na shule yetu. Shule yetu ni shule ya bweni na ni ya mchanganyiko yaani ni shule ya Wavulana na Wasichana.

Unatakiwa kusoma kwa makini maelezo yote katika fomu hii na kuyatekeleza kwa muda muafaka endapo hutaelewa wasiliana na uongozi wa shule kupitia namba zilizopo juu.

**KOZI YA UTANGULIZI**

Kabla ya kujiunga na kidato cha kwanza kutakuwa na utangulizi (pre form one) itakayoanza tarehe **25/09/2023** hadi **15/12/2023**. Hivyo mtoto wako anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe 25/09/2023** kuanzia saa mbili asubuhi.

**NB**

1. **Kozi hii ya pre form one ni ya lazima.Gharama ya kozi hii ni Shs 300,000/= Hii ni kwaajili ya chakula, malazi na ufundishaji.Malipo yafanyike kwenye akaunti ya shule ada kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.**
2. **Baada ya kukamilisha kozi maalumu ya pre form one, muhula wa kwanza wa kidato cha kwanza utaanza rasmi tarehe ……………….January, 2024. Ada ya shule kwa mwaka wa ni Tsh.1,800,000/=( Ada inaweza kulipwa yote kwa awamu moja hadi nne kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.**
3. **Malipo hayatarudishwa endapo mtoto hataweza kuripoti shuleni ama ataondoka shuleni kwa sababu yoyote.**

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya sekondari Medala ipo mkoa wa Iringa, wilaya ya Iringa, kata ya Idodi kilomita 70 kutoka Iringa Mjini kuelekea mbuga ya wanyama ya taifa Ruaha (**RUAHA NATIONAL PARK).**

**Jinsi ya kufika shuleni:** ukifika Iringa mjini unaelekea kituo cha basi cha Mlandege na kupanda basi linaloenda Idodi. Kabla ya kufika Idodi tarafani unashukia kituo kinaitwa **KITANDALU KIBAONI (Picha ya tembo)** kwa nauli ya **Tshs 5,000**. Muda wa mabasi kuondoka **Mlandege** ni saa tano, saa saba na saa nane mchana.

Shule hii ni ya bweni na ni ya mchanganyiko wa WAVULANA na WASICHANA wa DINI ZOTE. Shule inatambuliwa na WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA kwa usajili wa namba S.5613

**MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI**

i. Civics ii. English iii. Kiswahili iv. History v. Geography

vi. Basic Mathematics vii. Biology viii.Physics ix. Chemistry.

MEDALA HIGH SCHOOL P. O. Box 859 IRINGA-TANZANIA

CamScanner

# VITU AMBAVYO LAZIMA MWANAFUNZI AWE NAVYO

| NA | | | |
|---|---|---|---|
| | WAKATI WA PRE FORM ONE( Vifaa hivi mwanafunzi ataendelea navyo atakapoanza rasmi kidato cha kwanza ) | **Bei kw wote** | **WAVULANA /WASICHANA** |
| 1 | Truck suit mbili **zinapatikana shuleni** | 40,000/= | wote |
| 2 | Jezi,Tshirt na bukta 2 **Vinapatikana shuleni** | 30,000/= | wote |
| 3 | Begi la mgongoni la kubebea daftari **linapatikana shuleni** | 35,000/= | wote |
| 4 | Viatu vyeusi vya kamba visigino vifupi jozi 2 | Aje navyo | wote |
| 5 | Raba za michezo | Aje nazo | wote |
| 6 | Soksi jozi 5 **Zinapatikana shuleni** | 7500/= | wote |
| 7 | Saa ya mkononi | Aje nayo | wote |
| 8 | Mashuka manne-**Yanapatikana shuleni** | 32,000/= | wote |
| 9 | Chandarua pembe nne-**kinapatikana shuleni** | 8,000/= | wote |
| 10 | Kandambili jozi 1 | Aje nazo | wote |
| 11 | Tranka la chuma **Linapatikana shuleni** | 30,000/= | wote |
| 12 | Godoro ft 3 X 6 na mto –**Vinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 43,000** | 45,000/= | wote |
| 13 | Vibanio vya kuanikia nguo | Aje navyo | wote |
| 14 | Dawa ya meno,mafuta,sabuni ya kufulia na kuogea za kutosha | Aje nayo | wote |
| 15 | Taulo, mikanda miwili rangi nyeusi isiyo na kibanio kikubwa na vest | Aje navyo | wavulana |
| | Taulo, na kanga au kitenge au ijabu kwa waislamu kwaajili ya kwendea kuswali | Aje nvyo | wasichana |
| | Leso,kitambaa brush ya nywele,dodoki,tochi ya sola na nguo za ndani za kutosha na nguo ya kulalia (pajama) | Aje navyo | wote |
| | Taulo za kike za kutosha | Aje nazo | Wasichana |
| | Ndoo 1 ya usafi/kufulia **inapatikana shuleni** | **5000/** | wote |
| | Makufuli madogo mawili kwaajili ya Tranka | Aje nayo | wote |
| | Vyombo vya chakula (Sahani, kikombe,kijiko na chupa ya maji ya kunywa) Vinapatikana shuleni | 12,000/= | wote |
| | Stationary<br>Madaftari ya msomi 10, peni 10, Pencil HB 5,Ruler 1,Mathematical set, Box file 1 bei ni 3000 Vina[patikana shuleni | 20,000/= | wote |
| | Kuprint Majina kwenye Vifaa | 11,00 | wote |
| | Jumla ya fedha kwaajili ya mahitaji yanayopatikana shuleni | 273,500 | |

Kwa awamu hii ya pre form one, Mahitaji pamoja na gharama za kozi maalumu (pre form one)

Ni shs 573,000/= -(pre form one Shs 300,000/= -na mahitaji Shs 273,500/= italipwa kamaifuatavyo:

**BANK: NMB**

**NAMBA YA ACCOUNT:60510057830 ( MEDALA SECONDARY SCHOOL)**

MEDALA HIGH SCHOOL
P. O. Box 859
IRINGA-TANZANIA

CamScanner

**Wakati wa kuanza rasmi kidato cha kwanza,pamoja na mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu ambayo mwanafunzi atakuwa tayari,mahitaji yafuatayo yatahitajika.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Mashati meupe mikono mifupi(TomSato 2) | Aje nayo | Wote |
| 2 | Sare za shule zinapatikana shuleni | 15,000/= | **Wavulana**<br>Suruali 3,T-shirt 1,na sweta 1<br><br>**Wasichana**<br>Sketi 2, T-shirt 1, Sweta1, gauni-shaba dress 1 |
| 3 | Counter Books 12 Quire 3 **Zinapatikana shuleni** | 42,000/= | wote |
| 4 | Rimu 2 za karatasi kwa mwaka **zinapatikana shuleni** | 32,000/= | wote |
| 5 | Shati 1 nadhifu rangi yeyote mikono mifupi kwaajili ya kazi za nje. | Aje nalo | Wavulana |
| 6 | Dictionary (English/Oxford dictionary | Aje nayo | WOTE |
| | Jumla ya fedha kwa mahitaji yanayopatikana shuleni | 224,000/= | |

## ADA NA MICHANGO KWA MWAKA 2024
## ADA INALIPWA KWA AWAMU NNE KWA MWAKA MZIMA

| | JANUARI | APRIL | JULAI | SEPTEMBA |
|---|---|---|---|---|
| **ADA YA MASOMO,CHAKULA NA MALAZI** | **500,000/=** | **400,000/=** | **500,000/=** | **400,000/=** |
| | | | | |
| **FEDHA YA TAHADHARI** | **50,000/=** | | | |
| **JUMLA** | **550,000/=** | **400,000/=** | **500,000/=** | **400,000/=** |

**Kwa awamu hii ya kuanza rasmi kidato cha kwanza, mahitaji pamoja na ada awamu ya kwanza ni Tshs 774,000/=-(ada shs 500,000/- na mahitaj Shs 224,400/-na fedha ya tahadhari Shs 50,000/=)**

NB:

1. Ada ikilipwa hairudishwi
2. Mwanafunzi wa kidato cha pili na cha nne atawajibika kulipia gharama za mitihani ya taifa na utamilifu (mock) pamoja na masomo ya ziada itakapohitajika.

Malipo yote yafanyike benki kupitia akaunti ifuatayo:

**BANK: NMB**

**NAMBA YA AKAUNTI: 60510057830**

**JINA LA AKAUNTI: MEDALA SECONDARY SCHOOL**

Hati ya malipo (banki pay slip) iandikwe jina la mwanafunzi na kidato anachosoma na ifikishwe shuleni siku ya kuripoti au whatsap namba……0736313180 | 0735313180

MEDALA HIGH SCHOOL
P. O. Box 859
IRINGA-TANZANIA

**MALIPO MENGINE**

Kila mzazi anatoa fedha ya matumizi ya mwanafunzi (pocket money) kiasi cha 50,000/=ambayo itatumika kwa mahitaji ya sadaka (kanisani na msikitini) na mahitaji ya dharula kama ikitokea. Fedha hii itahitajia itakapoisha .( Ikumbukwe fedha hii si kwa mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu). Fedha hiyo iwekwe benki kwa akaunti namba ifuatayo:

**BANK: NMB**
**NAMBA YA AKAUNTI :6051007831**
**JINA LA AKAUNTI:MEDALA SECONDARY SCHOOL**

Hati ya malipo (bank pay in slip) iandikwe jina la mwanafunzi na kidato anachosoma ifikishwe shuleni siku ya kuripoti au kwa whatsapp namba……….

**MAHITAJI MENGINE**

AFYA:

- Kila mwanafunzi anatakiwa afanyiwe uchunguzi kamili wa afya na daktari iliyoambatanishwa iliyojazwa na daktari.
- Kila mwanafunzi aje na kadi yake ya bima ya afya .Kwa wasio na bima ya afya wanatakiwa kulipia shs 55,000/= -ili kusaidiwa kupata bima ya NSSF shuleni.(Gharama za matibabu kwa kipindi ambacho mwanafuzi atakuwa hana bima zitalipwa na mzazi.

**SUALA LA DINI**

Shule yetu haichangamani na dini yoyote na si nia ya shule kubadilisha dini au Imani ya mtu.Katika kuzingatia nidhamu ya shule hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kwenda kanisani au msikitini nje ya mazingira ya shule.Wanafunzi wote watawajibika kuhudhuria vipindi vya dini katika mazingira ya shule .

Hata hivyo ili kukidhi uhitaji wa ibada, shuleni kuendeshwe ibada. Kwa sasa kuna wahudumu kutoka madhehebu mbalimbali ya dini huja shuleni kuendesha ibada. Kwa sasa kuna wahudumu kutoka:

A) RC - Jumapili, kwa wanafunzi wakatoliki
B) KKKT - Jumapili kwa wanafunzi waprotestanti
C) TAG - Jumapili kwa wanafunzi wapentekosti
D) MSIKITINI - Ijumaa kwa wanafunzi waislam
E) SABATO - Jumamosi kwa wanafunzi wasabato

- Mwanafunzi wa kike kusuka nywele (Waislamu wanahusiwa kuvaa hijabu (Nyeupe)
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu au kitu chochote kinachohusiana na simupia asije na pasi.

**TAARIFA**

a. Jina la mwanafunzi………………………………………………Jinsia……………………
b. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………………………..
c. Shule aliyomaliza darasa la saba……………………………………………………….
d. Namba ya prem………………………………………………………………………….
e. Namba ya mtihani wa darasa la saba…………………mwaka aliohitimu…………………
Wilaya ……………………………………………mkoa………………

MEDALA HIGH SCHOOL P. O. Box 859 IRINGA-TANZANIA

## TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

a. Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………………………

b. Kazi yake……………………………………………………………………………………

c. Anuani yake…………………………………………………………………………………

**(Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi kutoka kwa daktari wa hospitari ya serikali (akichaguliwa kujiunga na shule) iletwe shuleni siku ya kuripoti shuleni.**

Naomba mtoto wangu ______________________________apatiwe nafasi ya kujiunga na kidato cha________________ katika shule yako. Natakuwa tayari kulipa ada na michango na kufuata masharti yote ya shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi______________________Tarehe_____________

## MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE

Tafadhali soma kwa makini maelekezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

1. Mzazi /mlezi ninakubali kwamba mwanangu atafuata sheria za shule,kanuni bna taratibu za shule kama zitakavyotolewa na mkuuB wa shule akitenda hivyo kwa mujibu wa mamlaka aliyonayo.
2. Mzazi /mlezi nakubali kwamba ,nitashirikiana na uongozi wa shule kuhalikisha kwamba kiwango cha juu cha nidhamu kinapatikana na kudumishwa.
3. Mzazi /mlezi nitafuatilia kikamilifu maendeleo ya mwanangu . Vile vile nitazungumzia maendeleo ya mwanangu na kufikia lengo hilo.LAZIMA nihudhurie mkutano wa wazazi kila ninapohitajika , kwamba kama maendeleo ya mwanafunzi yakithibitisha chini ya wastani wa **alama sitini (60)** nitashirikiana na walimu katika kutekeleza mikakati iliyopo ya kuboresha maendeleo ya kitaalam ya mwanangu.
4. Mzazi /mlezi ninakubali na nitawajibika kulipa ada wakati ,mara inapohitajika
5. Shule inaweza kuhitaji malipo kwa shughuli za ziada kama zinavyoweza kutokea kwa mfano ziara kimasomo n.k hivyo kama mzazi /mlezi wa mwanafunzi nakubali kushirikiana na uongozi wa shule katika kutekeleza adhima hiyo.
6. Mzazi au mlezi ninakubali kuwa mwanafunzi anaporipoti shule awe amelipa ada na michango yote kama ilivoidhinishwa kwenye jedwali la malipo. Mwanafunzi hatapokelewa endapo atakuwa hajakamilisha malipo yote ya muhula husika.
7. Mzazi/mlezi ninakubali kuwa hakutakuwa na marejesho au punguzo la ada kutokana na ugonjwa au sababu yoyote ya kutokuwepo shuleni pamoja na kumkatisha masomo mwanafunzi baada ya kuanza muhula wa masomo.
8. Mzazi /mlezi Ninakubali kuwa Taarifa yoyote inayomhusu mwanafunzi kwa mfano taarifa ya kufiwa itatumwa kwa mkuu wa shule na si kupitia kwa mwanafunzi .Taarifa kama hiyo itatolewa nje ya utaratibu uliotolewa hapo juu haitasikilizwa.
9. Mzazi/mlezi ninakubali kuwa mwanafunzi anatakiwa kuja shule na nywele fupi,asinyoe panki, au upara,hairuhusiwi kufuga ndevu wala kucha.Aidha anatakiwa kuwa safi na aoge mara kwa mara
10. Mzazi /Mlezi ninakubali kuwa mwanafunzi anatakiwa atunze mazingira ya shule katika hali ya ubora na usafi.

MEDALA HIGH SCHOOL
P. O. Box 859
IRINGA-TANZANIA

CS CamScanner

11. Mzazi/Mlezi ninakubali kuwa ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono ambazo lengo la kuendeleza elimu ya kujitegemea pamoja na kuimarisha afya ya mwili.
12. Ili mwanafunzi aweze kujifunza na kufaulu katika masomo yake mwanafunzi anatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu.

13.Anatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria zilizoambatanishwa nyuma ya fomu hii. Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa nauli pindi mwanafunzi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani.Ni wajibu wako mzazi au mlezi kugharamia hayo.

14.Mzazi au mlezi ninakubali kuwa mwanafunzi anatakiwa kushiriki michezo na lengo la kuleta mwema na kujenga miili yenye afya.

15.Kila mwanafunzi anaruhusiwa kufanya ibada kulingana na Imani yake ilimradi shughuli hizo zinaendeshwa kwa kufuata sheria za Nchi na ratiba ya shule.

16.Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule bila kibali maalumu kutoka kwa Mkuu wa shule

17.Shule haitatoa chakula maalumu kwa mwanafunzi tofauti na wengine.Aidha Mzazi/Mlezi unashauriwa umtafutie mahali amabapo ataweza kusoma na kupata huduma ya chakula kulingana na tatizo.

18.Mzazi mlezi hakikisha kabla ya mwanafunzi kupokelewa umekabidhi fomu iliyojazwa na daktari wa serikali juu ya afya ya mtoto katika ofisi ya malezi.

**MASHARTI MENGINE**

Mwanafunzi anapokuja shuleni awe amevaa tracksuit rangi kma zilivyoagizwa hapo juu.

- Mwanafunzi asije shuleni na nguo nyingine zaidi ya zile zilizoagzwa vinginevyo atarudishwa nyumbani.
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzake kuzuia uovu unaoweza kutokea katika chumba chao. Uharibifu wowote ule / ukibainika katika chumba wanafunzi wanaoishi katika chumba hicho wataadhibiwa wote, kwani wote watakuwa wameshiriki katika uharibifu wa mali ya shule . Mfano kuunganisha umeme kuchoma bweni, kuiba vitu.n.k
- Uharibifu wowote utakao sababishwa na mwanafunzi ni jukumu la mwanafuzi na mzazi/mlezi kugharamia matengenezo.

***KARIBU SANA MEDALA SEKONDARI KWA ELIMU NA MALEZI BORA***

MEDALA HIGH SCHOOL
P.O.Box 859
IRINGA-TANZANIA

***MKUU WA SHULE***

CamScanner